

DIRA NA DHIMA YA MAENDELEO YA WILAYA

Kuwa halmashauri bora kataika utoaji wa huduma endelevu za kijamii na kiuchumi kwa jamii na wadau wa maendeleo ifikapo2025 kwa kutoa huduma kiuchumi na kijamii kwa kutumia rasilimali zilizopo kikamilifu na kwa ufanisi kuititia utawala bora ili kuboresha maisha ya wananchi.

UTEKELEZAJI WA OPERATION YA ANWANI ZA MAKAZI NA POST KODI

- ❖ Wilaya ya Ileje katika utekelezaji wa zoezi la Anwani za Makazi na Posti Kodi iliweza kutambua Anwani 36,142 katia ya lengo la Anuani 35,562 sawa na asilimia 101.63 ya utekelezaji.
- ❖ Barabara zilizotambuliwa na kuingizwakwenye Mfumo wa NAPA ni 843 sawa na asilimia 103.3, huku jumla ya barabara 527 zimepewa majina na kusimikwa nguzo sawa na asilimia 64.6 ya lengo.
- ❖ Pia zoezi la uwekaji vibao katika nyumba limefanikiwa kwa kuweka vibao na kuandika namba za nyumba 33,818 sawa na asilimia 105.6 ya lengo la nyumba 32,000
- ❖ Aidha Wilaya ya Ileje itaendelea kuboresha miundombinu ya Anuani za Makazi na kuhuisha kila mara taarifa katika mfumo wa NAPA.

USHIRIKI WA ZOEZI LA KITAIFA LA SENSE YA WATU NA MAKAZI

- ❖ Wananchi wa Wilaya ya Ileje walishiriki kikamilifu katika zoezi muhimu la kitaifa la Sensa ya Watu na Makazi lilifanyika mnamo tarehe 23, Agosti, 2022, ambapo jumla ya kaya 34,042 na majengo 51,099 yalihesabiwa.
- ❖ Pia zoezi hilo liliweza kutoa ajira za muda kwa kwa makarani na wasimamizi 680 hivyo kunufaika kiuchumi.

HALI YA UCHUMI NA PATO LA MWANANCHI

- ❖ Katika kipindi cha 2021/2022 hadi 2022/2023 uchumi wa wilaya ya Ileje unaongezeka ukitegemea sana kilimo, ujasiliamali wa kati, mazao ya misitu na nyuki, ufgaji na biashara ndogondogo.
- ❖ Kilimo huchangia takribani asilimia 75 ya pato la wilaya wastani wa pato hilo kwa mwananchi wa Ileje ni Tzsh.2, 109,325.75 kwa mwaka

MAENEKO YA KIUTAWALA

- ❖ Wilaya ya Ileje ina Tarafa mbili 2 ambazo ni Bulambya na Bundali, kata 18, vijiiji 71 na vitingoji 316.
- ❖ Wilaya ina jumla ya madiwani wa kuchaguliwa 18 viti Maalum sita 6 wote wanatoka Chama cha Mapinduzi CCM ambacho ni chama Tawala hapa nchini.
- ❖ Aidha, wilaya ina jimbo moja la uchaguzi na mbunge mmoja wa kuchaguliwa kutoka Chama cha Mapinduzi CCM.
- ❖ Kwa mujibu wa muundo mpya wa kiutumishi halimashauri ina Divisheni tisa 9 na vitengo tisa 9.